# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1024

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-797-5

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA UALIMU KWA VITENDO STASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN 978-9987-09-797-5

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255-735041168/ +255-735041170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2023). *Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu (Elimu Maalumu)*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

Orodha ya majedwali ........ iv

Shukurani ........ vi

1.0 Utangulizi ........ 1

2.0 Malengo Makuu Elimu Tanzania........ 1

3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu Tanzania ........ 2

3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu ........ 2

3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu ........ 2

4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu ........ 3

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Elimu Maalumu ........ 3

6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4

6.1 Mkufunzi ........ 5

6.2 Mwalimu tarajali........ 5

6.3 Mzazi/mlezi ........ 5

7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6

8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6

9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji........ 6

10.0 Idadi ya Vipindi ........ 7

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7

Bibliografia........ 19

# Orodha ya majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 4

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu ........ 7

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji mwaka wa kwanza ........ 8

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji mwaka wa pili ........ 13

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

# Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, Taasisi inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya kusimamia kazi ya maboresho ya mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt.Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

## 1.0 Utangulizi

Somo la Ualimu kwa Vitendo ni la lazima katika Stashahada ya Ualimu Elimu ya Maalumu. Ujifunzaji wa somo hili utamwezesha mwalimu tarajali kumudu stadi za kuandaa somo, azimio la kazi, andalio la somo, shajara la somo na zana za kufundishia na kujifunzia. Pia, somo hili linalenga kumpa nafasi mwalimu tarajali kufanya mazoezi ya ufundishaji kwa kutumia mbinu na zana shirikishi, kutoa afua stahiki na kutoa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, kufanya upimaji na kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi, pamoja na kuchopeka masuala mtambuka na kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, ujifunzaji wa somo hili utamjengea mwalimu tarajali maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kuwa mbunifu, mnyumbufu na mwenye uwezo wa kuandaa mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mtoto.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu kwa Vitendo, Tanzania Bara. Pia, muhtasari unatoa maelekezo ya kumwezesha mkufunzi kuandaa mchakato wa ufundishaji kwa ufanisi ili kumwezesha mwalimu tarajali kujenga umahiri uliokusudiwa. Aidha, muhtasari unasisitiza ufundishaji na ujifunzaji utakaomwezesha mwalimu tarajali kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kujenga stadi za karne ya 21 zikiwemo ubunifu, mawasiliano, ushirikiano, fikra tunduzi na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Maalumu wa Mwaka 2023.

## 2.0 Malengo Makuu Elimu Tanzania

Malengo ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;
(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu Tanzania

### 3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu

Lengo kuu la elimu ya ualimu ni kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, na anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu ni kumwandaa mwalimu kuwa mahiri katika:
(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;
(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;
(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na
(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (classroom-based research).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu

Muhtasari wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu unalenga kumwezesha mwalimu tarajari:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kutambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (instructional leadership); na
(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (classroom-based research).

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Elimu Maalumu

Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Elimu Maalumu, una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyojitokeza katika jedwali namba 1.

**Jedwali Na. 1**: *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya elimu maalumu | 1.1 Kuchambua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa elimu maalumu |
| 2.0 Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika masomo ya elimu maalumu | 2.1 Kuandaa mazingira katika ufundishaji na ujifunzaji<br>2.2 Kuandaa zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>2.3 Kuandaa darasa salama, changamshi na jumuishi |
| 3.0 Kuwezesha ujifunzaji wa mwanafunzi katika masomo ya elimu maalumu kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | 3.1 Kusimamia darasa katika ufundishaji na ujifunzaji<br>3.2 Kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>3.3 Kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji<br>3.4 Kuchopeka matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji<br>3.5 Kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa darasa kubwa katika mazingira jumuishi<br>3.6 Kuratibu shughuli za ujifunzaji nje ya darasa<br>3.7 Kupima, kutathmini na kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>3.8 Kutoa ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na Ujifunzaji hutegemea ushirikiano baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi, jamii na wadau wengine wa elimu. Muhtasari huu unasisitiza majukumu ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi ili kufanikisha mchakato huo. Majukumu hayo ni:

### 6.1 Mkufunzi

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(b) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(c) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki;

### 6.2 Mwalimu tarajali

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaj zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ujifunzaji na ufundishaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo.

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

### 6.3 Mzazi/mlezi

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari umejikita katika kufanya vitendo kwa mwalimu tarajali, ikiwamo kuandaa somo, kuandaa zana za kujifunzia na kufundishia, kufanya mazoezi ya ufundishaji kwa kutumia mbinu na zana shirikishi, kufanya upimaji na kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi, kutoa afua stahiki pamoja na kutoa ushauri na unasihi. Vilevile, mwalimu tarajali atashiriki katika ufundishajionesho utakaofanywa na mwalimu mzoefu katika shule ya jirani. Mwalimu tarajali anapaswa kushiriki ufundishaji igizi chuoni (simulated teaching at college), ufundishaji wa darasa halisi chini ya uangalizi wa mkufunzi/mwalimu wa somo (teaching a real class under observation) na ufundishaji katika mazingira ya shule chini ya uangalizi wa mwalimu wa somo na mkufunzi (teaching in the school under supervision of a mentor teacher). Mkufunzi anashauriwa kumwongoza mwalimu tarajali kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia mbinu shirikishi wakati wa mazoezi ya ufundishaji na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji kulingana na mazingira aliyopo.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mwalimu tarajali anapaswa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira au kufaragua zana ambazo zitamsaidia mwanafunzi kujenga tabia ya udadisi, ugunduzi na kukuza fikra tunduizi kulingana na mahitaji aliyonayo. Vilevile, zitamwezesha mwanafunzi kutumia milango ya fahamu katika ujifunzaji. Baadhi ya zana hizo ni shime sikio, vioo kuza, fimbo nyeupe, abakasi, kikokotozi kinachoongea, stendi ya kusomea, kofia na hadubini. Zana hizi zimependekezwa katika jedwali la maudhui katika safu ya zana.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Elimu ya Awali utafanyika kwa kuzingatia vigezo vya upimaji wa maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujenzi wa umahiri. Mwalimu tarajali atapimwa kwa kufanya vitendo vya ufundishaji, ikiwamo kuandaa somo, kufaragua zana, kufanya mazoezi ya ufundishaji, kufanya upimaji endelevu na kutoa mrejesho.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Katika kuamua kiwango cha ufaulu wa mwalimu tarajali katika somo la Ualimu kwa Vitendo, upimaji wa mwisho utachangia asilimia thelathini (30%) na upimaji endelevu utachangia asilimia sabini (70%). Kwa upande wa upimaji endelevu alama za mtihani wa muhula wa pili mwaka wa kwanza itakuwa

asilimia 10%, kazimradi ya ufaraguzi 15% na ufundishaji igizi /kiduchu 20% Ufundishaji katika shule jirani 25%. Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia 50% na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafaulu, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli ya Upimaji | Mgawanyo wa Asilimia (%) |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhula wa Pili Mwaka wa Kwanza | 10 |
| 2 | Kazi Mradi ya Ufaraguzi | 15 |
| 3 | Ufundishaji igizi | 20 |
| 4 | Ufundishaji katika shule jirani | 25 |
| | **Jumla** | **70** |

### 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa somo la Ualimu kwa Vitendo unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi 6 kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Ualimu kwa Vitendo umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika Jedwali la 3 na 4. Maudhui haya yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni: Umahiri Mkuu, Umahiri Mahususi, Vigezo vya upimaji, Shughuli za kutendwa na mwanafunzi, vifaa/zana na Idadi ya Vipindi.

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji mwaka wa kwanza*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu Maalumu | 1.1 Kuchambua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu Maalumu | Kuaridhia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu Maalumu (aina, umuhimu, matumizi na changamoto) | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu Maalumu | Matini zinazohusu njia na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, video zenye maudhui ya mbinu ufundishaji na ujifunzaji | 10 |
| 2.0 Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa elimu maalumu | 2.1.Kuandaa mazingira katika ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kuchambua dhana ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji | Dhana ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji imechambuliwa | Muhtasari wa somo, Vitabu vya kiada na ziada ,mazingra halisi ya ujifunzaji, chati yenye kanuni za mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, matini mbalimbali zeye maudhui ya somo husika | 48 |
| | | (b) Kubaini kanuni za kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji | Kanuni za kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji zimebainishwa | | |
| | | (c) Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika miktadha mbalimbali | Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yameandaliwa kwa kuzingatia miktadha mbalimbali | | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kuandaa zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (a) Kutengeneza zana za ufundishaji na ujifunzaji | Zana za ufundishaji naujifunzaji zimeandaliwa | Makunzi yanayopatikana katika mazingira, vifaa saidizi, vitu halisi na mifano ya mafunzo | 31 |
| | | (b) Kuhifadhi zana za ufundishaji na ujifunzaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zimehifadhiwa | Seva na uhifadhi wa Mtandao, Kabati la digiti, karatasi na mikoba ya kazi, makabati, ratiba na kalenda, picha za zana za ufundishaji na ujifunzaji na vifurushi vya kuhifadhi zana | |
| | | (c) Kuandaa kivunge cha zana | Kivunge cha zana za ufundishaji na ujifunzaji kimeandaliwa | Boksi lenye kivunge cha zana, sanduku za kuhifadhi zana, vifuko na mifuko, makunzi, viandikio, mifano ya zana, ubao wa rangi, | |
| | 2.3 Kuandaa darasa salama, changamshi na jumuishi | (a) Kupanga darasa kwa kuzingatia mazingira na mahitaji ya wanafunzi | Darasa limepangwa kwa kuzingatia mazingira na mahitaji ya mwanafunzi | Samani, ramani na michoro ya darasa kwa kuzingatia mazingira na mahitaji ya wanafunzi, meza na viti kwa | 28 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kuzingatia mahitaji ya wanafunzi, maktaba na rasilimali za kujifunzia vifaa saidizi na zana za kujifunzia na kufundishia | |
| | | (b) Kupanga zana katika kona za ujifunzaji kulingana na mahitaji ya wanafunzi | Zana za ujifunzaji zimepangwa katika kona za ujifunzaji kulingana na mahitaji ya mwanafunzi | Zana za ujifunzaji (mguso, sauti, masikizi na masikizi maono), vitu halisi, kadi za mahudhui, rasilimali za kujifunzia, kona za ujifunzaji, nukuu za kusisimua, mipira ya rangi na sitika, karatasi za kuandika maswali na nyenzo za vitendo | |
| | | (c) Kuchochea utayari na ushiriki wa wanafunzi katika ujifunzaji | Utayari wa wanafunzi kushiriki umechochewa | Kadi za Kujifunzia, zana za Kujifunza za Kidijiti, Vifaa vya Kuonyesha na zana za kuchochea utayari wa kushirirki | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kuwezesha ujifunzaji wa mwanafunzi katika Elimu ya Msingi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | 3.1 Kusimamia darasa katika ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kubaini mahitaji ya kila mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji | Mahitaji ya kila mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji yamebainishwa | Dodoso la ubainishaji wa mahitaji ya mwanafunzi<br><br>Zana za ubainishaji wa mapema wa mahitaji ya mwanafunzi | 48 |
| | | (b) Kuhamasisha ushiriki wa mwanafunzi katika ujifunzaji | Ushiriki wa mwanafunzi katika ujifunzaji umehamasishwa | Video zenye maudhui ya kutumia kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji<br><br>Chati yenye kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji<br><br>Zana za ufundishaji na ujifunzaji zilizo shirikishi na jumuishi kama vile vitu halisi na mchoro/picha mguso | 48 |
| | | (c) Kutumia kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | Kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa zimetumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | | |
| | | (d) Kutumia mbinu na zana shirikishi, jumuishi na changamshi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | Mbinu na zana shirikishi, jumuishi na changamshi zimetumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (a) Kufundisha kwa kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi (ufundishaji igizi chuoni). | Somo limefundishwa kwa kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi | Zana na vifaa mbalimbali vya TEHAMA na teknolojia saidizi mfano tabuleti, kompyuta, runinga na projekta<br><br>Video zenye maudhui ya kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji | 46 |

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji mwaka wa pili*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (b) Kufundisha kwa kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi (ufundishaji wa darasa halisi na katika mazingira ya shule chini ya uangalizi wa mkufunzi na mwalimu wa somo) | Somo limefundishwa kwa kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi | Zana na vifaa mbalimbali vya TEHAMA na teknolojia saidizi mfano tabuleti, kompyuta, runinga na projekta<br><br>Video zenye maudhui ya kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji | 46 |
| 3.0 Kuwezesha ujifunzaji kwa mwanafunzi katika elimu maalumu kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | 3.3 Kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji | Masuala mtambuka yamechopekwa katika ufundishaji na ujifunzaji | Matini zinazohusu masuala mtambuka kama vile elimu jumuishi, maadili na ulinzi na usalama | 20 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 3.4 Kuchopeka matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji | TEHAMA imetumika katika ufundishaji na ujifunzaji | Zana na vifaa mbalimbali vya TEHAMA na teknolojia saidizi: tabuleti, kompyuta, runinga na projekta<br>Video zenye maudhui ya matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji | 28 |
| | 3.5 Kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa darasa kubwa katika mazingira jumuishi | (a) Kufundisha darasa kubwa na jumuishi kwa kutumia mbinu na zana shirikishi | Darasa kubwa na jumuishi limefundishwa kwa kutumia mbinu na zana shirikishi | Zana za kuona na kushika mfano vitu halisi na picha/ michoro mguso | |
| | | (b) Kubuni shughuli zinazohusisha matumizi ya mlango wa fahamu zaidi ya mmoja | Shughuli zinazohusisha matumizi ya mlango wa fahamu zaidi ya mmoja zimebuniwa | Video zenye maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji wa darasa kubwa na jumuishi | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 3.6 Kuratibu shughuli za ujifunzaji nje ya darasa | (a) Kupanga shughuli za ujifunzaji nje ya darasa | Shughuli za ujifunzaji nje ya darasa zimepangwa | Zana za ufundishaji wa shughuli za ujifunzaji nje ya darasa kulingana na shughuli husika<br>Mpango kazi, ratiba na kanuni za utekelezaji wa shughuli za ujifunzaji nje ya darasa<br>Orodha hakiki ya kutathmini shughuli za ujifunzaji nje ya darasa | 46 |
| | | (b) Kusimamia utekelezaji shughuli za ujifunzaji nje ya darasa | Utekelezaji wa shughuli za ujifunzaji nje ya darasa umesimamiwa | | |
| | | (c) Kutathmini shughuli za ujifunzaji nje ya darasa | Shughuli za ujifunzaji nje ya darasa zimetathminiwa | | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 3.7 Kupima, kutathmini na kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (a) Kutumia mbinu na zana za upimaji, ikiwemo TEHAMA, kutathimini maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi | Mbinu na zana za upimaji, ikiwemo TEHAMA, zimetumika katika kupima na kutathimini maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi | Sampuli ya zana za upimaji na maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi mfano hojaji, dodoso na mkoba wa kazi<br><br>Orodha hakiki ya kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi<br><br>Mwongozo wa uchunguzi wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi | 52 |
| | | (b) Kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi | Maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi yamefuatiliwa | Ripoti za maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi<br><br>Daftari la kumbukumbu za maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi | Mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi umetolewa | | |
| | | (d) Kutumia taarifa za matokeo ya upimaji katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji | Taarifa za matokeo ya upimaji zimetumika katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji | | |
| | 3.8 Kutoa ushauri na unasihi kwa mwanafunzi | (a) Kubaini mwanafunzi mwenye mahitaji ya ushauri na unasihi | Wanafunzi wenye mahitaji ya ushauri na unasihi wamebainishwa | Mwongozo wa ushauri na unasihi<br>Matini na video zenye maudhui ya kutoa ushauri na unasihi kwa mwanafunzi kuhusu masuala yanayoathiri ujifunzaji | 36 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutoa ushauri na unasihi kwa mwanafunzi kuhusu masuala yanayoathiri ujifunzaji | Ushauri na unasihi kwa mwanafunzi kuhusu masuala yanayoathiri ujifunzaji umetolewa | | |
| | | (c) Kutoa ushauri na unasihi kwa mwanafunzi kuhusu masomo na maisha ya kazi | Ushauri na unasihi kwa mwanafunzi kuhusu masomo na maisha ya kazi umetolewa | | |

# Bibliografia


Hakielimu. (2008). *Ripoti ya Utafiti wa Hali na Upatikanaji wa Elimu kwa watoto wenye Ulemavu Tanzania*.HakiElimu.

International Disability Alliance. (2020). *Ripoti ya Shirikisho la Kimataifa la Walemavu*. UKAid.

Muzale, H. R.T. (2009). *Changamoto za mawasiliano kwa viziwi Tanzania. African Journal Online.* Vol.72 N0.1.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2016). *Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundisha Elimu ya Awali.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2018). *Moduli ya Kufundisha Masuala Mtambuka Darasa la I na II: Programu ya Mafunzo Endelevu ya Mtaala kwa Walimu Kazini*.Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2018). *Moduli ya Kufundiaha Masuala Mtambuka: Darasa la I na La II.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). *Muhtasari wa Somo la Elimu Jumuishi kwa Mwalimu Tarajali*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu ya Elimu Tanzania. (2019). *Muhtasari wa Somo la Elimu Jumuishi kwa Waalimu Tarajali:* Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Taasisi ya Elimu Tanzania.

The United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.(2022).*Muhtasari wa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu 2021-2022.* UNESCO.